# EE BWANA MUNGU WANGU

Zab. 30 : 1, 3, 5, 10-12 (K) 1

Rogers K.J
2007
Dodoma

**Wimbo wa Katikati**
**Jumapili ya 3 ya Pasaka, Mwaka C**




1. Ee Bwana nitakutukuza kwa maana umeniinua,
   Wala hukuwafurahisha adui za-ngu juu yangu
   Umeniinua nafsi yangu, Ee Bwana, kutoka kuzimu
   Umenihuisha na kunitoa, miongoni mwao washukao shimoni.

2. Mwimbieni Bwana zaburi, Enyi watauwa wake//
   Na kufanya shukrani kwa kumbukumbula utakatifu wake,
   Maana ghadhabu zake ni za kitambo kidogo
   katika radhi yake mna uhai, huenda kilio huja kukaa usiku
   Lakini asubuhi huwa furaha.

3. Ee Bwana usikie unirehemu, Bwana uwe msaidizi wangu,
   Uligeuza matanga yangu kuwa machezo;
   Ulinivua gunia, ukanivika furaha,
   Ee Bwana Mungu wangu nitakushukuru milele.